

**RASIMU YA MAAZIMIO YA MKUTANO WA SABA WA WADAU WA KAHAWA 26-27,
MAY 2016**

No	Azimio	Mhusika
1	Kuwepo na mikakati ya kutatua changamoto za masoko ya kahawa yenye lengo la kuongeza ushindani kwenye soko la kahawa, kuimarisha soko la ndani na kumsaidia mkulima kupata bei nzuri.	TCB
2	TaCRI ishirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kufuatilia upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya utafiti wa kahawa katika Wilaya ya Tarime-Mara na Buhigwe-Kigoma.	TaCRI, LGAs, TCB
3	Serikali kupitia Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi itimize ahadi yake ya kuchangia shilingi bilioni mbili kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa ambayo haijatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita.	WKMU, TCDF, TCB
4	Kuwepo na mkakati wa kuhamasisha matumizi ya mbolea, kuanzisha mashamba darasa ya matumizi sahihi ya mbolea na kuimarisha huduma za ugani.	LGAs, TCDF
5	Serikali iendeele kutoa ruzuku kwenye zao la kahawa	WKMU
6	Benki ya Maendeleo ya Kilimo ianze kutoa huduma za mikopo kwenye zao la kahawa kama inavyofanya kwenye mazao mengine na ialikwe kuhudhuria mkutano ujao wa wadau.	TCB, TADB
7	Randama ya Makubaliano ya wadau ya mwaka 2011 ifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia mapendekezo yaliyowasilishwa kwa kuzingatia viwango vya uchangiaji vilivyokubalika awali. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo: Utafiti – 0.75%, Mfuko – 0.2%, Mnada wa kahawa – 0.2%.	TCB, TCDF, WKMU, TaCRI
8	Mapendekezo ya wadau ya kuongeza viwango vya uchangiaji katika Mfuko, Utafiti na Bodi yafanyike baada ya utekelezaji wa tamko la Serikali la kupunguza kodi na makato katika tasnia ya kahawa, na kwa utaratibu maalumu utakao kubaliwa na wadau kwa kuitisha mkutano mkuu maalumu kusaini randama ya makubaliano.	TCB, TCDF, WKMU, TaCRI

9	Kuwepo na mikakati mahususi ya kuwezesha vijana kushiriki katika mnyororo wa thamani wa zao la kahawa.	TCB, LGAs
10	Sheria ya Tasia ya Kahawa ifanyiwe marekebisho kuruhusu wakulima wa kahawa kuuza kahawa ya madaraja yote nje ya nchi.	TCB, WKMU
11	Mpango wa Mfuko wa kuwawezesha wakulima kupata mbolea (Pembejeo) uboreshwe kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau kabla ya kuanza kutekelezwa.	TCDF, WKMU
12	Maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo cha kahawa yabainishwe, yapimwe hati miliki zitolewe na masharti ya uendelezaji yasimamiwe.	TCB, WKMU, LGAs, ARDHI
13	Wadau wa kahawa watekeleze mkakati waliojiwekea wa kuzalisha miche milioni 20 kwa mwaka na kuhakikisha kwamba kila mkulima anapanda miche mipya.	TCB, TaCRI, LGAs
14	Serikali iweke mazingira mazuri ya kuendeleza sekta ya kahawa.	WKMU, TCB, LGAs, WVB